
NAILINDA
NDOTO
Yangu
GETRUDE AUGUST

Toleo la kwanza

Hakimiliki © 2023
Getrude August
Baruapepe: getrudeyaugust1990@gmail.com
WhatsApp: +255 768 190 060

Ubunifu wa jalada na sanifu ya ndani ya kitabu
DL Bookstore
+255 787 163 013, authors@dlbookstore.com
www.dlbookstore.com
Arusha, Tanzania

ISBN 978 9912 41 025 1

Hatimiliki, Haki zote zimehifadhiwa hairuhusiwi kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutumia aina yoyote ya elektroniki. Kwa kutoa upya nakala ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi.

# YALIYOMO

Shukrani........................................................ v

Sura Ya Kwanza........................................................ 1

Tunu Za Mtoto........................................................ 1

Sura Ya Pili........................................................ 7

Sababu Za Ndoto Kufa........................................................ 7

Sura Ya Tatu........................................................ 27

Haki Za Watoto........................................................ 27

Sura Ya Nne........................................................ 31

Haki Za Watoto Wazazi Wanapotengana........................................................ 31

Sura Ya Tano........................................................ 39

Malezi Ya Watoto Katika Msingi Wa Kibiblia........................................................ 39

Sura Ya Sita........................................................ 49

Thamani Ya Watoto........................................................ 49

Hitimisho........................................................ 57

*Nukuu zote za maandiko katika kitabu hiki zimetolewa katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV).*

# SHUKRANI

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya, uzima na maono ya kuandika kitabu hiki. Namshukuru Dickson Mtalaze kwa kuniongoza na kuwa nami kuanzia mwanzo wa kuandika kitabu hiki hadi tamati. Nawashukuru wazazi, jamaa na marafiki kwa kunitia moyo katika safari yangu ya uandishi.

Ninawashukuru nyote.

*Mithali 29:18*

*"Pasipo maono watu huacha kujizuia; bali ana heri mtu yule aishikaye sheria."*

# SURA YA KWANZA

## TUNU ZA MTOTO

Kila mtoto ana tunu nne ambazo zinaposimamiwa ipasavyo huzaa matunda mema. Tunu hizo ni maono, kusudi, kipaji na ndoto.

### Maono ni Nini?

Maono ni picha au taswira inayojengeka ndani ya akili ya mtu juu ya mambo yanayomtokea au anayopaswa kuyatenda. Kwa maana nyingine, maono ni mawazo ambayo mtu huwa nayo ndani ya akili yake kuhusu namna anavyofikiri mambo fulani yanavyotakiwa kuwa au anavyotakiwa kuyafanya. Kwa maana hiyo, kabla Mungu hajafanya kitu katika maisha ya mtu humpa mtu huyo picha ya jambo analotakiwa kuja kulifanya ili mtu huyo aweze kutumika naye kutimiliza jambo hilo. Hayo ndiyo maono ya Mungu.

Mchungaji David Oyedepo ameelezea katika kitabu chake cha Understanding Vision kwamba, *'Understand that you are born to fulfill a particular course. A discovery of that course is what is called a vision.*

*Vision, therefore, can be defined as the unfolding of a divine plan as it is related to a nation, a group of people or an individual".* Kwa tafsiri isiyo rasmi anamaanisha kwamba, *"Elewa kwamba umezaliwa kutimiza kusudi fulani. Ugunduzi wa hilo kusudi ndicho kiitwacho maono. Vilevile, maono yanaweza kutafsirika kama kujifunua kwa mpango wa Kiungu juu ya nchi, kundi la watu au mtu mmoja."* Kwa maana rahisi ni kwamba maono ni vile unavyoweza kuwa kesho kutokea leo. Maono hayahusiki na mambo yaliyopita bali mambo yajayo.

Dkt. Myles Munroe aliwahi kusema, *"I think the greatest gift God ever gave man is not the gift of sight but the gift of vision. Sight is a function of the eyes, but vision is a function of the heart."* Kwa tafsiri isiyo rasmi, *"Nafikiri zawadi kubwa ambayo Mungu amewahi kumpa mwanadamu si kuona bali zawadi ya maono. Kuona ni kazi ya macho lakini maono ni kazi ya moyo."*

Watoto wanapokuwa wadogo huwa na ndoto au maono makubwa na mazuri juu ya kesho yao. Lakini katika hali isiyotarajiwa, kadiri wanapokua watoto wengi huenda tofauti na maono yao.

Je, hayo maono au hizo ndoto huwa zinakwenda wapi wanapokuwa wakubwa?

Wanasaikolojia wanasema kuanzia wakati mtoto anapozaliwa mpaka anafikia umri wa kujitambua hupitia hatua mbalimbali za ukuaji kama ifuatavyo:

> **Hatua ya kwanza** ni pale tangu mtoto anapozaliwa hadi anapofikisha umri wa miaka 11. Katika kipindi hiki watoto hufanya vitu kwa ajili ya kujifurahisha tu. Hivyo, katika wakati huu siyo lazima hiyo michezo anayocheza au mambo anayofanya ndiyo atakuwa anayafanya maisha yake yote au ndiyo maono yake. Kwa wakati huu huwa hawajitambui vyema hivyo hufanya mambo pasipo malengo yoyote.

**Hatua ya pili** ni pale mtoto anapofikisha umri wa miaka 11 hadi miaka 17. Katika hatua hii mtoto anaanza kufanya vitu anavyopenda kwa sababu anakua ana uelewa wa kile anachofanya. Mtoto anakuwa anajua anapenda nini na kitu gani hapendi, ana uwezo kwenye kitu gani n.k. Hapa mtoto anaweza kujizatiti kwenye kile kitu anachopenda.

**Hatua ya tatu** ni kuanzia miaka 17 hadi miaka 20 na kuendelea. Hapa mtoto anakuwa anajitambua vyema na kuwa na uelewa mpana wa mambo mbalimbali, hivyo mtu anakuwa huru kufanya maamuzi na kuchagua kitu kimoja anachopenda kukifanya na akakiishi hicho katika maisha yake. Hivyo wazazi, walezi na walimu wana nafasi kubwa ya kutambua ndoto au maono ya mtoto mapema zaidi kwa sababu wao ndiyo huwa karibu na watoto katika hatua mbalimbali za ukuaji.

Turejee katika Biblia; Mungu alipomuumba mwanadamu, alimpa mamlaka na uwezo wa kuitawala dunia na vitu vyote. Alimpa uwezo huo wa kumiliki, kutawala na kuona vitu kwa upeo mkubwa tofauti na viumbe wengine. Ujio wa kila mtu hapa duniani ni mpango kamili wa Mungu. Hakuna mtu aliyeumbwa pasipo mpango au kusudi kutoka kwa Mungu. Hili huanza kuonekana kwa mtoto akiwa mdogo, ambapo huonesha kiu na matarajio makubwa ya kuwa aina fulani ya mtu katika siku za usoni. Ari na ndoto za watoto ni uthibitisho wa kuwa kila mtu ameumbwa kukamilisha kusudi fulani.

Watoto wanapoanza kukua huwa na matarajio makubwa na ndoto kubwa, lakini kadiri siku zinavyosonga mbele ndivyo ndoto au maono hayo hujidhihirisha au hupungua au kupotea kabisa na kubaki kama historia.

Kile kitu ambacho mtoto anakuwa amekiona ndani yake (maono) huwa kinaweza kuwa kweli endapo kitamwagiliwa ili kimee na kuzaa matunda, pia kitalindwa kisiharibike au kupotea.

Nimewahi kufanya mahojiano na watu wengi, nikawauliza walikuwa na ndoto gani walivyokuwa watoto. Mara zote nilikuwa nikishangaa walipokuwa wakinieleza vitu vikubwa.

Watu hawa walikuwa na ndoto kubwa walipokuwa watoto kwa sababu kwa kawaida watoto huwa wanaamini kwamba kila kitu kinawezekana. Ni rahisi kwa mtoto kuwaza kuwa rubani, waziri, rais, mhandisi, mcheza mpira, daktari, mwanamuziki, mwalimu au yeyote mkubwa katika jamii kwa kuwa huwa hana neno **KUSHINDWA** katika akili yake, bali ni **KUSHINDA** tu.

Ndiyo maana tulipokuwa wadogo, tulipoona magari tulikuwa tunasema ni magari yetu au wakati mwingine tulikuwa tunawaambia wazazi wetu watununulie ndege kisha wakatuahidi kufanya hivyo, tulifurahi na kuamini kwa kuwa katika fikira zetu tulikuwa tukiamini kila kitu kinawezekana. Hivyo kila mtoto huwa na ndoto na maono ambayo anaamini yanaweza kutimia.

## Kusudi Maalum ni Nini?

Kusudi la kufanya jambo lolote hutangulia kabla ya jambo husika kuumbwa au kufanyiwa kazi. Kwa maana hiyo, kabla Mungu hajamuumba mwanadamu, alishajua kwamba huyo mwanadamu atakuja duniani kufanya kitu gani. Kwa hivyo, ndani yake humuwekea uwezo na nguvu ya kufanya kitu hicho kifanikiwe. Kuna watu wameumbwa kwa kusudi la kutatua matatizo fulani hapa ulimwenguni. Kwa mfano, mtu aliyegundua ndege ambayo inabeba abiria na mizigo kutoka bara moja hadi lingine. Mtu huyu aliumbwa kwa kusudi hilo la kuja kutatua tatizo la uchukuzi ambalo huenda lilisumbua vichwa vya watu kwa miaka na miaka. Maono makubwa kama hayo huandaliwa na Mungu mwenyewe kabla mtu hajazaliwa.

Kwa sababu mwingine amegundua ndege, haina maana sisi ambao hatujagundua ndege hatujaumbwa kwa makusudi. Hapana. Nasi

tumeumbwa kwa makusudi yetu. Kwa mfano, kusudi la kuumbwa kwangu ni kuandika kitabu hiki unachokisoma sasa. Na wewe msomaji kama ulikuwa hujui kusudi la maisha yako, anza sasa kulitafuta.

## Je, Kusudi la Mwanao ni Lipi?

Watoto wetu wameumbwa na Mungu kwa makusudi fulani. Hawapo hapo duniani kwa bahati mbaya, wala hawajaja kuongeza mizigo, bali kuna mizigo wamekuja kuipunguza, kwa kuwa Mungu hatuwazii mabaya hata tuseme anaumba watu kwa makusudi ya kutuangamiza.

Unaweza kujiuliza mwanao kaumbwa kwa kusudi la kugundua au kufanya nini, kwa kuwa unadhani karibia kila kitu kimeshagunduliwa na wengine. Dunia ni kubwa sana, na bado vitu vingi havijagundulika, hivyo, mwanao huenda ameumbwa kwa kusudi la kuvigundua.

Mungu amemuumba kila mtu awe mtawala kwenye jambo au eneo fulani. Maana yake ni kwamba kila mtu ana kitu ndani yake cha kukitawala, na hicho kitu ndicho maono. Maono hayo yanatakiwa kulindwa, kutunzwa na kukuzwa ili yatimie na kuwa halisi.

Maono yanatakiwa kulindwa na kukuzwa ili yatimie, kwa kuwa unaweza kuyalinda lakini ukashindwa kuyasimamia na kusiwe na maana yoyote.

Unatakiwa usiwe mwoga. Hata kama kuna hofu ndani yako, ishinde kwa kuamua kufanya bila kujali utafanikiwa au utakwama. Kuna hofu huja ili kukuonya na nyingine huja ili kukuzuia kuvuka upande wa pili wa kufanya mambo makubwa na mazuri kwa ajili ya dunia yako. Hofu zimewafanya watu wajutie kwenye maisha yao yote. Mwandishi Mark Twain aliwahi kusema kuwa, *"Miaka ishirini (20) kutokea sasa utakuja kujutia kwa vitu ambavyo hukufanya na ulitamani*

*kufanya."* Sasa, ili kesho usijute yakupasa leo hii ufanye na kujipa changamoto. Na wazazi/walezi mnapaswa muwasaidie watoto kutimiza ndoto zao ili wasije wakajuta huko mbele.

## Kipaji ni Nini?

Kipaji ni uwezo wa asili anaozaliwa nao mtu wa kufanya jambo fulani kwa namna ya kipekee. Ni uwezo ambao unaweza kuishi ndani ya mtu bila kupotea na kadiri unavyozidi kutumika ndivyo huzidi kuimarika. Kipaji cha mtu kinaweza kutambulika kupitia fikira zake na matendo yake katika kutenda au kujaribu kufanya mambo mbalimbali. Mfano wa vipaji ni kama kuchora, kuimba, kuogelea nk.

## Ndoto ni Nini?

Ndoto ni tamanio la ndani la kufanya jambo fulani au kuwa mtu fulani. Kuwa na ndoto ni kutengeneza picha ya matamanio unayoyotaka kufikia au mambo unayoyataka kufanya na kupata katika maisha yako.